Kutoa Presha

Asante, Ndugu Ruddell. Nina furaha sana kujua nina mwana katika Injili. [Ndugu mmoja anasema jambo fulani—Mh.] Naam. Vema, barabara. Hilo ni jambo zuri. Naam, hakika ninamthamini Ndugu Ruddell. Nami ni—ninaamini Paulo wakati mmoja alikuwa na mwana aliyeitwa Timotheo. Alimwita mwanawe katika Injili.

2 Na kama sina hakika, huyu Flossy Ford, ndivyo alivyokuwa? [Dada Flossy anasema, "Ndiyo."—Mh.] Loo, jamani! Flossy, mimi . . . Imekuwa muda mrefu. Naam, imekuwa ni muda mrefu. Ninakumbuka, wakati nilipokuwa mvulana, mimi pamoja na ndugu yake, Lloyd, tulikuwa tukizunguka huku na huko pamoja. Naye alikuwa akioka keki kubwa, unajua, nasi tungekwenda kule na kula mpaka karibu tuumwe, kwa kuila.

3 Ninakumbuka wakati mmoja walinialika kwao, Lloyd aliniomba. Nasi . . . Flossy alikuwa ameoka. Alikuwa ni mtoto mdogo tu wakati huo. Alikuwa ameoka keki kubwa, na—nasi tukaila mpaka tusingeweza kula. Nikawazia, "Sasa, nitakaa usiku kucha pamoja na Lloyd." Kwa namna fulani usiku unaingia, unajua, ndipo ni—nikaamua kwamba ilinibidi tu niende nyumbani. Na kwa hiyo ni—nikatimua mbio kushuka barabarani, huku nikiogopa mno, nikijaribu kwenda nyumbani.

4 Na ni—ninamkumbuka baba yake. Mama yako angali hai, nadhani. Vema, hilo ni sawa. Na mambo mengi yametukia tangu siku hizo. Naam. Sisi tupo hapa sasa, sote wawili tukiwa na umri wa makamu, mababu. Vema, lakini, ipo Nchi ambako hatutazeeka kamwe. Unaona? Ninafurahi sana kujua, Flossy, ya kwamba unaitafuta Nchi hiyo, na hakika utaipata.

5 Na Jim, Jim ana hali gani? Yeye ananinii . . . Naam, ninakumbuka jambo hilo. Jim, huyo ni mume wake. Nami ninamkumbuka vizuri. Na niliwajua watoto wachache. Kwa namna fulani sisi, kwenye wakati huo, nilikuwa nimeingia kwenye huduma, wakati walipofunga ndoa, na watoto wao wakikua. Na kwa namna fulani tuliachana, unajua, mmoja kwa mwingine.

6 Ninamwona Ndugu Lloyd mara moja moja, ninampigia makelele, barabarani. Wamenipikia milo mingi. Nami nimeninii . . . kama ndugu na dada halisi.

7 Sasa, nina furaha sana kuona ya kwamba jitihada ya kwanza ya Ndugu Ruddell ilikuwa hapa katika mahali hapa; kubadilisha, alipoanza, kubadilisha nyumba ya pombe kuwa nyumba ya Bwana. Hilo ni jambo zuri sana.

8 Na, hakika, mnajua, kama wakati mwingine kama unaweza kuona jambo lolote kabla, unajua, na—na ndipo hilo linalifanya

kuwa zuri zaidi. Kwa hiyo tungeweza kuona mbele ya kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani ya mvulana huyu. Naye alikuwa mwenye haya. Mimi pamoja na baba yake, pale, tulikuwa tukifanya kazi pamoja miaka kadhaa iliyopita. Nami nilijua baba yake alikuwa ni hodari wa kupata vitu, kwa hiyo mbona hiyo isiwe hivyo kwa mvulana huyu? Najua alikuwa na mama mpendwa. Kwa hiyo, alizaliwa kwa haki, kwa hiyo ilibidi kuwe na jambo zuri nyuma yake, unaona. Na shauku hiyo moyoni mwake, kumtumikia Bwana! Kilindi kinapoita Kilindi, hapana budi kuwe na Kilindi cha kujibu wito huo. Na nina furaha sana kumwona Ndugu Ruddell akisonga mbele.

9 Kundi hili zuri sana la watu hapa. Na ni majaliwa makubwa sana kwangu, usiku wa leo, kuja hapa, na kulizungumzia kundi hili la watakatifu ambao wanasafiri hapa. Sisi si ninii . . . Hapa si mahali petu pa kuishi, unajua. Sisi ni wasafiri. Ndivyo tulivyo. Hatuko nyumbani.

10 Ninakumbuka, Dada Ruddell, jinsi ambavyo ungekuja pamoja naye na kuketi pale. Naye angeinamisha kichwa chake. Nawe ulikuwa na ujasiri mwingi. Hakika walikuwa nao. Mkewe aliamini mumewe—mumewe angehubiri Injili. Na kwa hiyo akiwa na mke mzuri namna hiyo, na baba na mama, na wote wakimwombea, ilibidi jambo fulani litukie, Ndugu Ruddell. Kwa hiyo hili hapa. Nami ninaomba, Ndugu Ruddell, ya kwamba hapa patakuwa tu ni ma—mahali pako pa kusimama, ambapo utaruka ufikie vilele vya juu kabisa, kwa ajili ya utukufu wa Injili.

11 Ninajua ya kwamba Ndugu na Dada Ruddell, Max pale, wangefurahia jambo hilo, usiku wa leo. Jinsi ningetaka kumwona Billy Paul amesimama mimbarani. Nami ninatumaini kuishi siku moja kumwona Joseph amesimama mimbarani. Na hilo ni zuri sana.

12 Jitihada zetu na shida basi tulizo nazo, kuwalea watoto wadogo kupitia utineja na kadhalika, hilo linatufanya tujisikie vizuri basi. Unaangalia nyuma na kuona mvi katika nywele za baba yako, na kadhalika. Kumbuka, baadhi ya—baadhi ya matendo yako mabaya yaliweka huo pale. Na hiyo—hiyo ni kweli.

13 Vema, inafaa kuwa hapa. Nami nimepwelewa kidogo na sauti. Nimekuwa nikihubiri. Mimi na Ndugu Gene Goad tulifanya ziara ndogo, jana, na tukaenda kule chini. Na samaki walikuwa wakiguguna. Na—na kwa hiyo tulikuwa na wakati mzuri, nilikuja nimechelewa. Na kwa namna fulani tulitoka majini, tumeshikwa na baridi kidogo, lakini ninatumaini mtanivumilia.

14 Sasa, tunajitayarisha kuondoka kwenda kwenye kampeni ya msimu wa kiangazi, kampeni ya kama siku tisini. Tunatarajia kurudi tena mwishoni mwa Agosti, tarehe moja ya Septemba.

Nasi tunaenda huko sasa. Juma hi—hili, nitaanzia huko Green Bay, Michigan, nirudi Chicago kwa ajili ya Jumapili alasiri, kwenye shule ya sekondari ya juu, mkutanoni. Nitahubiri kwenye mkutano wa kwanza wa Wafanyabiashara Wakristo huko Green Bay, Wisconsin. Na halafu, kutoka hapo, niende Chicago. Na halafu Jumatatu, nitakuwa Chicago, kwenye m—mkutano mkubwa, mkutano wa kimishenari kwa ajili ya Ndugu Joseph Boze. Na ndipo nirudi nyumbani, niende huko kusini, Southern Pine, North Carolina, na nishuke niende South Carolina. Kisha hadi kule Cow Palace South Gate, Los Angeles. Tuna makanisa arobaini na kitu ya Oneness yanayoifadhili mikutano hiyo. Ni mara ya kwanza ambapo Oneness wamepata kuifadhili mikutano yangu.

15 Halafu kutoka hu—huko nipande, California kupitia Oregon, kuingia Canada. Na kutoka huko, kuingia Anchorage, Alaska. Kisha nirudi tena mwishoni mwa mwaka huu, ambapo Ndugu Joseph Boze anaenda Kenya, Tanganyika, Urban, huko Afrika, Afrika Kusini, kupanga mikutano baadaye kwenye msimu wa kupukutika majani.

16 Sasa, kusema nina mwongozo wa kwenda kwenye moja ya sehemu hizi, sina. Lakini ninajisikia ya kwamba ninapaswa kuwa nikipanda Mbegu mahali fulani, nikifanya chochote niwezacho kwa ajili ya ule Ufalme.

17 Na sasa hebu tuinamishe tu vichwa vyetu tena kwa ajili ya neno jingine la maombi. Si kwamba hatujaombewa, bali ningetaka tu kumwomba Bwana anisaidie hapa sasa, ili anipe Maneno kwa ajili yenu.

18 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunakaribia kiti Chako cha neema, katika Jina la Bwana Yesu, aliyetupa ruhusa na kutuagiza tuje, nasi tutapewa mambo tunayoomba, tunapokaribia. Sasa, tusingeomba, hata kidogo, kusimama kwenye hukumu Yako. Lakini tunataka kusimama kwenye Kiti cha Rehema, kusudi tupate rehema, tukikiri ya kwamba tumekosea. Wala sisi si wazima. Bali tunajitoa wenyewe, Bwana. Hakuna kitu tunachoweza kutoa, ni maombi tu ya Bwana wetu Yesu, na agizo, ya kwamba Yeye alisema jambo hili, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Tunaamini jambo hilo. Yeye alituagiza tuje, tuombe lolote katika Jina Lake, tungepewa. Tunaamini hilo.

19 Juu ya msingi wa imani yetu, tunakuja, tukiomba ya kwamba Wewe ulibariki kanisa hili, na ndugu yetu mpendwa, Ndugu Ruddell, na familia yake, na familia zote zilizowakilishwa hapa.

20 Nilipoangalia na kumwona Bibi Morris hapa, usiku wa leo, na kuwazia juu ya siku zilizopita. Na, Mungu, kama nilivyomwambia, mambo mengi yametukia, na hatari nyingi,

kazi ngumu, na mitego. Tayari umetupitisha kwenye hayo, Bwana, na tumaini letu liko Kwako, ya kwamba twende kwenye mwisho wa safari, katika Wewe.

21 Bariki mahali hapa. Weka Jina Lako hapa ndani, Bwana, na uwape kile kilicho bora kabisa kilichochaguliwa kwa ajili ya mahali hapa. Jalia uovu, kama vile ndugu mmoja alivyoomba, usiku wa leo, hapa, kijana mwanamume huyu, alivyoomba ya kwamba ungeondolea mbali vizuizi vyote. Tujalie, Bwana. Jibu ombi lake.

22 Waponye wagonjwa walio miongoni mwetu. Tupe wokovu kwa nafsi ya wale wanaoona njaa na kiu ya haki. Na sasa, Bwana, takasa sauti na ninii—na jitihada za mtumishi wako asiye na faida. Na bariki Neno Lako, na jalia lisirudi bure. Lakini liwe, jalia liwe hivyo, ya kwamba litatimiza lile lililokusudiwa. Jalia Roho Mtakatifu ayatwae mambo ya Mungu, usiku wa leo, na kuitia nguvu mioyo yetu, kutoka aliye mkubwa sana hata aliye mdogo sana. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

23 Sasa, asubuhi ya leo, nilihubiri muda mrefu. Na sikujua kuhusu kuhubiri. Nilikuwa tu kwa namna fulani nikifundisha somo la shule ya Jumapili. Siku moja, nilifundisha kwa muda wa saa sita. Haitakuwa namna hiyo, usiku huu, nina hakika.

24 Lakini nina fungu dogo tu la maneno hapa, ambapo ningetaka kusoma Maandiko machache, kwa maana ninajua Maneno Yake hayatashindwa. Yangu huenda yakashindwa. Yangu yanaweza yakashindwa. Na nitajaribu kuweka neno langu sawa na Lake, na kuchukua Neno Lake; kuchukua neno langu, kujenga somo kwenye Neno Lake, tunapolitumia kama fungu la maneno.

25 Ninataka kusoma sehemu mbili, usiku wa leo. Ninataka kusoma katika Kitabu cha Methali, katika mlango wa 18, na kifungu cha 10, kwa sehemu moja. Na sehemu nyingine, ninataka kusoma Isaya 32:2. Sasa katika Methali 18:10

> *Jina la* B*WANA ni ngome imara; mwenye haki huikimbilia,* akawa *salama.*

26 Na katika Kitabu cha Isaya, mlango wa 32, kifungu cha 1 na cha 2.

> *Tazama, mfalme atamiliki kwa haki, na* mkuu *watatawala kwa hukumu.*
>
> *Na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo, na mahali pa kujisitiri na dhoruba; kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu.*

27 Na sasa kutoka kwenye fungu la maneno, ninataka kutumia hili kama fungu la maneno, ku. . .*Kutoa Presha*. Hilo ni fungu la ajabu, "Kutoa presha." Nilichagua hili kwa sababu ya kwamba, kabla ya kuja kwenye mkutano, daima mimi hukazana

kuomba, na kujitahidi kumtafuta Bwana. Sio kusimama mbele ya kusanyiko lolote, dogo ama kubwa, mmoja hadi milioni moja, ingekuwa ni kusimama pale sio nipate kuonekana wala kusikika, bali kufanya jambo fulani kumtukuza Bwana wangu, kwa hiyo, nikiyaona mahitaji ya watu.

28 Wala nisingekuja hapa nipate kusikika, kwa maana mimi sifai kusikilizwa; sauti mbaya, si mtu mwenye elimu. Wala kamwe sidumu kwenye somo langu; ninarukaruka kila mahali, toka Mwanzo hadi Ufunuo. Wala mimi—mimi si m—m—msemaji hodari, bali ninampenda Bwana. Wala si—siwezi kumpenda Kristo mpaka kwanza niwapende watu Wake. Unaona? Sina budi kuwapenda watu Wake. Kwa hiyo kama ninawapenda watu Wake, basi ninampenda Yeye.

29 Halafu ninataka kuwa kama alivyofanya. Ninataka ku—kufanya kusudi langu liwe kusudi lile lile alilokuwa nalo, na, hilo lilikuwa ni, daima akijaribu kufanya mema, kumsaidia mtu fulani.

30 Na tukiona siku hii tunayoishi, na tukijua ya kwamba kanisa hili hapa lina mchungaji mzuri . . .

31 Sasa, sisemi hilo kwa utani, ninasema hilo kutoka moyoni mwangu. Kama nilisema jambo lolote tofauti, ninge—ningekuwa mnafiki. Nami—nami ninaamini ya kwamba kanisa hili lina mchungaji ambaye angetetea Kweli, kwa vyovyote vile. Ninaamini hivyo. Hayo ndiyo matumaini yangu kwa mwa—mwanangu. Na ni—ninaamini jambo hilo. Na mimi . . . Naye ni mjasiri awezavyo kuwa. Na ninyi . . . Ninaamini yeye ni mtu wa heshima, mtu mtakatifu, aliyetumwa kutoka kwa Mungu, akiwa na huduma kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Naye anahubiri sehemu ile ile ya Neno ambayo ninahubiri, hiyo ni kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, jinsi tu lilivyoandikwa. Nami ninapenda jambo hilo. Hakuna kupatana, anadumu tu na Neno, nami napenda jambo hilo.

32 Lakini basi nilifikiri, kukiwako na mtu kama huyo, kwangu kwenda nyuma ya mimbara yake, akiwa angali ni kijana mwanamume, ningesema nini ambacho kingelisaidia kusanyiko lake? Kwa sababu, hiyo ndiyo sababu alitaka nije huku. Yeye ni mchungaji wa kondoo, na anachunga kondoo wake. Naye angefikiri labda sasa, ili kubadilisha kidogo kwa namna fulani, huenda akawa na kitu cha kuwasaidia watu wake. Naye anawapenda. Anayajali masilahi yenu. Mchana na usiku, atakwenda wakati wowote, mahali popote, asaidie kufanya lolote awezalo. Vema, huyo—huyo ni mtumishi halisi wa Mungu.

33 Na kama alivyosema, alisema alinikera, ama kunisumbua, ama kuniudhi, ama chochote kile. Yeye hafanyi jambo hilo. Hilo linanifanya nimpende zaidi sana, wakati anaposhikilia kunialika, maana, hilo, ninapenda hilo, maana ana imani. Inaonyesha yeye asingenileta mbele ya kondoo wake kama

nilifikiria nitawadhuru. La. Hakuna mchungaji angefanya hivyo. Kwa sababu, yeye angefikiri ningefanya yaliyo mema. Na ni ninii . . . yeye . . . Ni baraka kuu anayonipa hapo anaponiomba nije. Nami ninapenda makusudi ya—yake, yaani "Shikilia mpaka litakapotukia." Huyo ni m—mtu wa imani, nami ninapenda hilo.

34 Kwa hiyo basi niliwazia, "Ningelihubiria kusanyiko hili kitu gani?" Nikawazia, "Vema, labda wamefunzwa vema katika kila kitu, hapana shaka." Lakini kuna presha juu ya watu siku hizi. Na presha hiyo haina kikomo, wala mipaka yoyote ya kimadhehebu. Haina mipaka ya umri. Haimjali mtu. Iko kwa vijana na wazee, wazuri na wabaya. Iko juu ya kila mtu: presha.

35 Tunaishi katika wakati wa fadhaa, wasiwasi wa akili. Kila mtu anatimua mbio *huku*, na kuenda *kule*, wala haendi kokote. Ni kwa wakati tu wa aina hiyo. Na ninajua kanisa hili lingekuwa linateseka nayo, kama vile ilivyo kila mahali panateseka nayo. Maskani imevamiwa nayo, kila mahali, ulimwengu mzima.

36 Ni siku ya presha. Haraka, haraka; haraka, haraka; mtu unaharakisha kisha unangojea. Mtu unaendesha gari maili tisini kwa saa, na ndipo unafika nyumbani kwa ajili ya chakula cha jioni, na kungojea saa mbili mpaka kiwe tayari. Hiyo ni kweli. Ni—ni wakati. Na katika harakati hizi na mwendo wa kasi, zinakuingiza katika wasiwasi wa akili. Mke akisema kitu kidogo kinyume, unataka kupasuka: hasira. Mume akisema jambo fulani, utachapua mguu wako na kumwambia aingie chumbani. Unaona? "Vema, sasa, mume wangu, sitaki kuzungumza nawe. Ondoka uende huko nje."

37 "Mke, loo, nina wasiwasi sana." Unaona? Kwa nini? Kuna nini? Unaona?

38 Haya yote, pamoja, wasiwasi huu unaongezeka, basi matokeo yake ni: kufanya kosa fulani, na kutenda vibaya. Hiyo ni kweli. Sasa, itawafanya maskini kufanya hivyo. Itawafanya watu wa tabaka la kati kufanya hivyo. Itawafanya matajiri kufanya hivyo. Itawafanya wabaya kufanya hivyo. Itawafanya walio wazuri sana kufanya hivyo. Na itawafanya walio wema kufanya hivyo. Kwa sababu, ni wasiwasi, msongo, uliolundikana. Huna budi kuulipua mahali fulani. Unaona? Usipofanya hivyo, utalipua bwela.

39 Sasa, tunaona jambo hilo. Unalundikana siku zikisonga mbele. Hebu mzungumzie bosi wako, kama unafanya kazi, "Loo, *nanii*!" Na kama ukimzungumzia mtoto, "Njoo hapa ndani!"

"Mama! Mimi ni . . . " Unaona?

Haya basi. Inalundikana. Looo! Jamani! Unaona? Unajisikia kama unaenda kunininii . . . kichwa kitang'oka. Ninajua. Ninayo, kila siku, kwa hiyo ni—ninajua inachomaanisha. Inalundikana. Nilikuwa . . .

40 Niliwazia juu ya jambo hili, hivi majuzi usiku. Nilikuwa kwenye hospitali fulani. Na mchungaji wetu, nilifikiri alikuwa mgonjwa, bali alikuwa tu amechoka. Kapiga mbio, mbio, mbio, mbio, mpaka akachoka tu. Na baadhi yao walisema, walipiga simu, walipiga simu ofisini kule chini, wakaomba kama ningeenda kuwaona wagonjwa kwa niaba yake. Vema, nilikuwa nimeshughulika siku nzima, na wahudumu kutoka mahali mbalimbali. Nikasema, "Naam." Vema, nikaenda kuwaona wagonjwa wake.

41 Basi nikaenda kwenye hospitali fulani. Nao wakanipa jina la mwanamke fulani, na ninii—na namba ya mahali alipokuwa. Nikaenda kwenye chumba hiki. Nikamwendea mama yule. Na i—ilikuwa yapata dakika kumi na tano, ishirini kabla ya wakati wa kuwapokea wageni. Kwa hiyo nikaenda pale na kumwambia mama huyo nilikuwa mhubiri na ningetaka kumwona mwanamke fulani, fulani. Akaniangalia usoni. Naye alikuwa akifanya jambo fulani. Akageuka, kwanza, na kusema, "Ati unataka nini?"

Nikasema, "Ningetaka kujua mahali mama *nanii* alipo kwenye wodi hii."

Akasema, "Sijui mimi."

Nikasema, "Vema, nilipewa namba fulani, mahali fulani, nami nikawazia ningeuliza kwanza."

Kasema, "Vema, kama una namba, nenda kaione."

"Asante."

Ninashuka ninaenda kule na kuketi kwenye mlango wa wodi. Nikasema, "Je! yupo mama hapa ndani, jina lake Nanii?"

"La."

Vema, nikarudi nikaangalia kwenye kijikaratasi changu. Hapo ndipo kiliposema. Kwa hiyo nikarudi, na huyo mama alikuwa amesimama pale. Nikasema, "Hiyo namba ilikuwa siyo."

"Ati ulisema jina lake ni nani?" Nikasema. Kasema, "Yeye hayuko kwenye orofa hii."

"Asante." Nikasema, "Nitapanda orofa ya juu basi."

Kwa hiyo, nikapanda kwenye chumba cha pili. Nami nikaenda kwenye. . . Kwanza, kulikuwako na daktari ameketi kwenye dawati, na ameketi pale, akijikuna kichwa. Kasema, "U hali gani?" Akaangalia juu tu, akaangalia chini.

Vema, nikawaza, "Afadhali nimwache peke yake."

Kwa hiyo nikaenda mbele kidogo kwenye safu, ndipo nikamkuta mama mmoja kwenye dawati, nesi. Kasema, "Samahani."

Kasema, "Unataka nini?"

Ndipo nikasema, "Je! kuna mama hapa jina lake ni *nanii*?"

Naye akasema, "Sijui." Nami nikasema . . . Akasema . . .

Nikasema, "Nilipaswa kupata chu—chumba namba 321 ama 221." Ndipo nikasema, "Nilienda kwenye chumba kile, wala hakukuwako na mtu kule. Na mama huyo akasema, 'Hakuna mtu hapa anayeitwa hivyo, kwa hiyo,' kasema, 'labda ni orofa ya juu.'"

Naye akasema, "Vema, basi mbona usiende kwa mbili . . . 321 basi."

Nikasema, "Asante."

Nikashuka nikaenda kwenye 321, Mimi . . . ama mia mbili ishirini . . . 321. Nikasema, "Yupo mama fulani hapa ndani anayeitwa *Nanii*?"

"La."

Kuna mama aliyekuwa amelala pale, kasema, "Alikuwa upande huo mwingine wa chumba hiki, upande huo mwingine wa chumba huko—huko kwingine, thelathini na moja."

Nikasema, "Asante, mama."

Nikaenda kule, nikasema, "Je! mama *Nanii* yupo hapa?"

"La. Walimtoa. Yeye yuko kwenye orofa ya chini."

Nikawazia, "Loo, jamani!"

Nikarudi chini tena. Mimi—mimi . . . Naye . . . Walinipa namba ya chumba hicho. Ndipo nikashuka kwenda kwenye orofa ya chini, na nikaangalia kote . . . Niliogopa kwenda kwenye dawati hilo tena. Kwa hiyo nikaangalia huku na huko, nikijaribu kupata nambari hiyo ya chumba. Nami ni—nikaangalia, wala nisingeweza kuipata.

Wana sehemu ndogo na kadhalika zilizojengwa kwenye hospitali hii. Kwa hiyo huyu hapa daktari huyu anashuka, akiwa na stethoskopu yake mkononi mwake, na mkoba wake. Na kamwe sikuwa nimepata kuona mtu aliye na urefu wa futi nne na upana wa futi nne, bali alikuwa karibu awe hivyo . . . Alikuwa akitembea pale. Nikasema, "Habari za jioni, bwana. Waweza kuniambia mahali chumba nambari *fulani* kiko?"

Akasema, "Panda *hivi* ukatokee *kule*."

Nikasema, "Asante kwa kunipasha habari." Hiyo ni kweli. Alisema, "Panda *hivi* ukatokee *kule*."

Basi nikasema, "Asante!" Nikawazia, "Sijafika mahali popote bado."

42 Niliangalia nyuma na kulikuwa na mama ambaye kwa namna fulani alikuwa akionekana mpole amesimama kwenye lile dawati tena. Nikamwendea, na nikasema, "Habari za jioni."

Akasema, "U hali gani?"

43 Nikasema, “Mama, nimechanganyikiwa kabisa.” Nami nikamwelezea hadithi yangu. Nikasema, “Kuna mama fulani hapa mahali fulani ambaye atafanyiwa upasuaji asubuhi, naye yuko karibu kufa. Mimi ni mhudumu, na mchungaji wetu huko aliko asingeweza kuwatembelea, nao wakanipa namba hii.”

Akasema, “Hebu kidogo, Ndugu Branham, nitatafuta kujua.” Akaninii . . .

“Vema, namshukuru—namshukuru Bwana.”

Aliweka kila kitu chini akaenda huko, na akapata . . .

“Loo,” akasema, “naam, Ndugu Branham, yeye yuko kwenye chumba *fulani*, kwenye mkono wako wa kushoto, papo hapo.”

44 Nikasema, “Asante, sana.” Nikageuka na kuangalia.

45 Nikawazia, “Jambo ndilo hilo, kutoa mvuke,” kila mtu. Unakuwa tu ni wakati wa—wa fadhaa. Kila mtu ameshinikizwa sana. Hana wakati. Na hiyo inalundikana kufikia mahali inapovunjilia vitu mbali. Inawafanya watu kukasirika, wakati wanapolipuka, na—na kusema mambo usiyotaka kusema.

46 Sasa, kila mtu ana hatia ya jambo hilo. Nina hatia. Nyote mna hatia. Sisi, sisi hufanya mambo chini ya presha ambayo vinginevyo tusingeyafanya, kwa hiyo kuna ninii—kuna presha ya ziada inayoumbika siku hizi. Ninaamini . . . Kabla sijaenda mbali zaidi, huenda nikasema jambo hili. Ninaamini ni adui anayeshuka na kusukuma. Ninaamini ni ibilisi.

47 Nasi tunajua Kuja kwa Bwana kumekaribia. Nayo Biblia ilisema, katika siku za mwisho, ya kwamba, “Ibilisi angezunguka-zunguka kama simba angurumaye.” Na kama angeweza kukuweka chini ya presha, ukiharakisha, ukipitia haraka juu ya jambo fulani, utafanya maamuzi ambayo usingeyafanya kama ungeketi na kuwazia jambo hilo.

48 Yapata miaka mitatu iliyopita, nilikuwa kwenye ziara ya kuwinda, nami nilikuwa na kiongozi wa Kihindi. Nami hu—huwinda haraka sana. Ni ninii tu, huyo ni mimi tu, unaona, mmoja wa wenye kulundika presha.

49 Kwa hiyo ni—nilikuwa nikiwinda na Mhindi huyo, nami nikaruka nikatoka juu ya farasi. Na kulikuwa na kulungu mlimani, nami nikaanza kupiga kona. Huyo mzee wa Kihindi alikuwa amenipita umri kwa miaka kumi hivi. Alikuwa tu akihema, akinifuata. Nikasema, “Hima, chifu. Hima!”

Kasema, “Haraka mno! Haraka mno!”

Nikawaza, “Loo, vema!” Nikasema, “Hima, na tuanze.”

50 Akasema, “Ni haraka mno!” Nikapunguza mwendo, gia ya pili. “Ni haraka mno! Haraka mno!” Nikafikia kutembea. “Mbio mno!” Loo, jamani!

Nikasema, “Chifu, kulungu yuko huko juu!”

Akasema, “Yeye huishi huko. Alizaliwa huko.”

Nikasema, “Naona hiyo ni kweli.”

“Yeye huishi huko, alizaliwa huko.” Akasema, “Mhubiri huwinda haraka sana, anawashtua wanyama wote wanakimbia.” Kasema, “Fanya kama Mhindi. Waendee hatua moja, waangalie mara tisa.”

51 Vema, sijui ni gia ya jinsi gani ingenibidi kuingiza, kushuka kwenda kule? Ambako, nilikuwa mbioni, nikipanda mlima. Akasema, “Waendee mara moja, kisha waangalie mara tisa. Angalia kila upande, juu ya kila kitu, mara tisa, kabla hajachukua hatua nyingine.” Loo, jamani! Lakini, unaona, yeye hana haraka. Niliwazia jambo hilo.

52 Na maskini mama yangu mzee wa thamani, ambaye yuko Utukufuni usiku wa leo; mtu fulani alisema, “Kwa nini usivae ua jeupe leo, ikimaanisha mama yako amekufa?”

53 Nikasema, “Mama yangu hajafa. Mama yangu yu hai.”

Na basi ningevaa jekundu, ndipo watu watasema, “Nilidhani mama yako alikufa.”

Kwa hiyo kusudi nisiwachanganye, na kulundika msongo zaidi, niliachilia hayo yote. Unaona? Yeye hajafa. Amelala. Yuko pamoja na Kristo.

54 Na basi wakati huu wenye wasiwasi na fadhaa tunaoishi! Nanyi mnajua, katika yote haya, madaktari hawana jawabu, maana wanasumbuliwa nalo, pia. Hawana jawabu. Hawajui la kufanya.

Unasema, “Loo, daktari, ni—ni—niko karibu kukilipua kichwa changu. Sijui la kufanya. Mimi . . . ”

“Vema,” yeye angesema, “Na mimi pia. Vema, hakuna unaloweza kufanya.” Angekupa dawa ya kukutuliza. Hiyo ikiisha kupungua nguvu, una wasiwasi mwingi kuliko ulivyokuwa nao mara ya kwanza; ni kama mlevi, akinywa kinywaji kingine, apate kupunguza ulevi wake. Unaona? Kwa hiyo hu—huwezi kufanya jambo hilo. Hakuna jawabu. Hawana.

55 Lakini, Mungu ana jawabu. Hilo ndilo tunalotaka kuchukua, kuzungumza habari zake, kupata jawabu. Mungu ana jawabu. Yeye ndiye jawabu. Kristo ndiye jawabu la kila shida tuliyo nayo. Sasa, tutazungumza habari Zake sasa.

56 Sasa, katika Agano la Kale, kulikuwa na wakati ambapo mwanadamu angeweza kulimbikiza msongo kule nyuma, na hapo ilikuwa ni wakati alipofanya uovu. Kama alimwaga damu isiyo na hatia, vema, basi alitoroka. Kwa sababu, mara yule mtu aliyemwua, ama kosa alilofanya; huyo mtu aliyemkosea, baadhi ya watu wake wangemtafuta mpaka wampate, na hapo angemwua. “Ilikuwa ni jino kwa jino, na jicho kwa jicho.” Na, unaona, mtu hakuwa na mahali pa kusimama.

Kama alifanya jambo bila kukusudia, na, kwa kweli, hao watu wasingeamini hilo, vema, ilimbidi kutoroka. Kwa maana mara—mara alipofanya hivi, basi ndu—ndugu wa mwanamume huyu, ama mwanamke, yeyote yule, walianza kumtafuta. Basi walipompata, "Ilikuwa ni jino kwa jino, na jicho kwa jicho." Hivyo ndivyo walivyoishi.

57 Na kwa hiyo asingeweza kusimama mahali popote. Alikuwa mkimbizi. Hakujua la kufanya, na alikuwa mbioni.

Mfano halisi wa leo hii. Nafikiri hilo ndilo linalosababisha presha kubwa namna hii. Tuko mbioni. Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu, wakijua wamekosea. Wakijua Kuja kwa Bwana kumekaribia, na presha inalundikana. Nao wako mbioni; kilabu cha pombe, chumba cha kucheza karata, anasa, dhambi, upotovu wa uadilifu, chochote kile, kutoa msongo. Wanasikiliza televisheni, utani mchafu, chochote kile, kuondoa msongo. Wako mbioni. Kuna jambo fulani lililo karibu kutukia. Wanalijua, nao wanakunywa pombe kupindukia, pamoja na anasa na chochote kile, mbioni.

58 Wanajua kuna jambo lililo karibu kutukia. Ulimwengu unazungumzia habari zake. Tunajua ya kwamba jambo fulani liko karibu kutukia. Ulimwengu huu unaweza ukalipuliwa kabla ya mapambazuko. Kila taifa limejaa wasiwasi. Kwa nini?

59 Wakati mmoja nilikuwa huko Afrika, nami nilikuwa nikiangalia kondoo akila. Ilikuwa ni mwana-kondoo, loo, kondoo wa makamu. Na maskini jamaa huyo alikuwa akila kwa utulivu sana, na kwa ghafla akashikwa na wasiwasi. Naye angeuma; angeangalia kote. Angeuma. Ambapo, alikuwa ametulia. Nilikuwa nikimwangalia. Alionekana mtulivu sana. Nikawaza, "Mahali pale si ni patulivu? Mwangalie maskini jamaa yule." Mchungaji aliyekuwa akiwachunga alikuwa ameenda zizini, amerudi; mwenyeji, mtu mweusi.

60 Basi nikamwangalia maskini jamaa huyu. Na muda si muda akashikwa na wasiwasi. Nikawazia, "Maskini jamaa yule mdogo ana shida gani?" Nilikuwa nikimwangalia, bila shaka, kwa darubini. Naye akashikwa na wasiwasi sana. Angeangalia *huku* na *huko*. Akaanza kulia. Hakujua la kufanya. Nikawazia, "Ni kitu gani kilimfanya maskini jamaa yule mdogo kushikwa na wasiwasi, kwa ghafla?"

61 Sasa, alikuwa kwenye uwanja mdogo wa malisho. Lakini kule nyuma kabisa, niliona kitu fulani kikiinuka na kushuka chini tena, kama nusu maili kutoka kwake. Simba alikuwa akimnyemelea, huku amejificha vizuri kwenye majani. Na maskini jamaa huyo mdogo, kitu fulani ndani yake kilikuwa kikijilundika kufikia mahali ambapo alijua kulikuwa na hatari mahali fulani. Asingeweza kuiona. Bali yule simba alikuwa amepata harufu ya huyo kondoo, naye ilimbidi aharakishe sasa ampate, kabla mchungaji hajampata, hajamwondolea mbali.

62 Kwa hiyo basi, nikiwa ninamwangalia, wasiwasi ulikuwa umeongezeka. Na huko mbali simba huyu alikuwa akimnyemelea, kwa makini sana. Hata hivyo, ko—kondoo huyo asingeweza kumwona huyo simba, bali kuna kitu fulani tu ndani yake kilichomwambia ya kwamba hatari imekaribia.

63 Hivyo ndivyo ilivyo leo hii, ya kwamba kuna kitu fulani ndani ya watu, kinachowafanya kujua jambo fulani liko karibu kutukia. Tunajua jambo hilo. Mkristo analijua. Ulimwengu unalijua. Mlevi analijua. Mcheza karata analijua. Mfanyabiashara, serikali, U.M., wote wanajua kwamba jambo fulani liko karibu kutukia. Limesababisha wasiwasi.

64 Wanawake, akina mama, sigara moja baada ya nyingine! Ninawaangalia wakija shuleni. Wanapitia kwenye ujia wetu pale. Inanibidi kuwachunga watoto wangu na mbwa wangu. Kwenye eneo la maili ishirini; wanaendesha mwendo wa maili sabini kwa saa, wanawake wakiwapeleka watoto wao shuleni. Sigara mkononi mwao, ukining'inia nje ya mlango mmoja, wakiwakemea watoto wao, na kule chini na kufunga breki upesi, halafu, ama tairi, na kuacha tairi barabarani. Na hawa hapa wanarudi tena. Niliona upepo ukiwapeperusha watoto wanne ama watano moja kwa moja kutoka barabarani, hivi majuzi, wa mama mmoja mwenye fadhaa. Anaenda wapi? Kuna nini? Kipindi fulani cha televisheni kinaendelea, labda kinakuja, alitaka kukiona.

65 Lakini, jambo ndilo hilo, wasiwasi. Kuna kitu kinachousababisha. Walikuwa ninii, hawakufanya hivyo. Kitu fulani kinakaribia. Mauti na maangamizi yako njiani yakija huku. Hayako mbali sana. Kitu fulani kinakaribia.

66 Sasa, katika Agano la Kale, Mungu akiona, katika baadhi ya shida hii, ilitokea kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, kama wewe huna kosa, na huna hatia, Mungu hukufanyia njia.

67 Sasa, kama mtu alimwua mtu, kwa makusudi tu, alikusudia kuua, alipotea. Asingeweza kuja mahali hapa. Lakini kama aliua kwa bahati mbaya, hakutaka kufanya hivyo, basi kulikuwa na mji wa kukimbilia. Mmoja ulikuwa ni Ramothi-Giliadi. Na miji minne, nafikiri, Yoshua aliweka miji hii ya kimbilio.

68 Sasa, sasa, watu wangeweza kuja kwenye mji huu wa kukimbilia kama alikuwa amefanya kosa kwa bahati mbaya. Hakukusudia kufanya hivyo. Angekuja kwenye huo mji wa kukimbilia, na aende kwenye lango. Mlinzi wa lango angemwuliza kwa nini anakuja, wazo lake la kuja ni nini. Ndipo kesi yake ikatetewa. Na hapo kesi yake ilipotetewa hapo langoni, na mtu huyo aonekane hana hatia, hakufanya makusudi, ndipo mtu huyo aliingizwa mjini, kama mahali pa kukimbilia. Ndipo adui asingeweza kumpata.

Na kama alisema uongo na alifanya makosa, kisha aingie katika mji wa kukimbilia, ingawa alikuwa ameshikilia pembe

za madhabahu, adui wake alikuwa na majaliwa na haki ya kumkokota kutoka kwenye hiyo madhabahu na kumwua, naam, bwana, kwa kuwa alikuwa na hatia, alikusudia, na ilimbidi apate adhabu.

69 Sasa, kuna kitu fulani kilichoambatana na jambo hilo. Hakika, mtu huyo angekuwa na wasiwasi, jamani, labda, watu dazani moja nyuma yako. Mahali fulani, kila mwamba, kila kilima, kila kichaka, adui, mtu fulani alikuwa anamvizia. Alikuwa na wasiwasi. Ndipo basi mara alipofika kwenye mji huo, angeweza kutoa presha. Alikuwa salama. Alikuwa sawa, maana kulikuwako na mahali palipoandaliwa kwa ajili yake. Njia iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya mtu huyo asiye na hatia, asije akauawa, bali angeachiliwa asiuawe, kwa kuwa alifanya jambo hilo kwa bahati mbaya, sasa, kama hakukusudia kufanya hivyo.

70 Sasa, kama alikusudia kufanya hivyo, vema, i—ilimbidi kustahimili hali za mambo. Bali hawezi kuachiliwa kama alifanya hivyo makusudi.

71 Na kuna matabaka mawili ya watu siku hizi. Hebu niseme jambo hili. Wapo wanaume na wanawake ulimwenguni leo, Ndugu Ruddell, ambao kweli hawataki kufanya mambo haya wanayofanya. Wapo wanaume na wanawake ulimwenguni leo, ambao hawataki kutenda dhambi. Ninawahurumia. Hawataki kufanya jambo lolote baya, bali wanalifanya. Wanasukumwa kwenye hilo. Sasa, kuna mahali kwa ajili ya mtu huyo anayetaka kufanya haki. Kuna mahali pa kutolea hiyo presha. Ni kweli. Ila wapo wengine ambao hawajali.

72 Hivi majuzi, ndugu mmoja, Hickerson, aliniletea pasi kutoka kwa mlinzi wa jela la serikali huko...huko La Grange, Kentucky, ya kuingia, kwenda kuvua samaki. Nami nikakutana na mvulana mweusi mbali huko kutoka Louisville. Naye akaniambia...Nikasema, “Mtu mwenye sura nzuri, mwenye akili kama wewe, unafanya nini huku?”

73 Akasema, “Vema,” kasema, “kasisi, hivi ndivyo ilivyokuwa.” Kasema, “Si kosa la mtu yeyote ila ni langu.” Kasema, “Wakati mmoja ni—ni—nilikuwa upande wa Bwana.” Jina lake lilikuwa ni Askofu. Akasema, “Wananiita ‘Askofu Mtakatifu’ kwa sababu ninamtumikia Bwana.” Akasema, “Mimi na mke wangu, tu—tulimpata msichana mdogo.” Kisha akasema, “Kuna wakati mmoja nisingeweza kuvumilia kamwe, kwa hiyo nikaenda tu na ulimwengu, nikamwacha Bwana.” Kasema, “Nilikuwa na baba na mama Wakristo.” Halafu akasema, “Nilitumika miaka minne katika nchi za ng’ambo, huko Korea,” kwamba alikuwa katika vita vingapi, nishani za heshima na kadhalika. Akasema, “Lakini huko nje mambo tuliyofanya ni kwenda tu kwenye madansi na kadhalika. Nikachanganyikana na kundi baya.

74 “Ndipo siku moja, wavulana wawili walikuja na kusema, ‘Askofu, tunataka kwenda kwenye Quaker Maid, kununua vyakula. Je! utatukimbiza kule?’”

Kasema, “Mke wangu alikuwa ndio kwanza aniitie chakula cha mchana. Nami nikasema . . . Kasema, aliniita mle ndani, kasema, ‘Mpenzi, usiambatane nao. Hakuna jambo jema katika watu hao. Tunapaswa kuwaacha, turudi kanisani tena.’”

Naye akasema, “Vema,” kasema, “Nikasema, ‘Ninachukia wasininii . . . Hao vijana wanataka vyakula.’ Kasema, ‘Nachukia kutowapeleka.’ Naam, kasema, ‘Nitawaachia gari langu.’”

“Kasema, ‘Usifanye hivyo. Wataliharibu kabisa.’ Kisha kasema, ‘Wakimbize kule haraka, ndipo urudi basi.’”

75 Kasema, “Niliwakimbiza kule, ndipo nikasimama kwenye mahali pa kuegeshea magari.” Kasema, “Nilikuwa nimeketi pale, nikingojea. Na kwa ghafla, king’ora kikalia, na kila kitu. Na hawa hapa hao vijana wanakuja, kila mmoja wao akiwa na bastola mkononi mwao. Ndipo nikafunga mlango. Nikasema, ‘Hamtaingia humu ndani.’” Ndipo mmoja wao akampiga sana kichwani, na kumsukuma nyuma, akatupa bunduki yake. Akasema, “Hunichukui.”

Akaitupa bunduki hiyo ndani, kasema, “Iwapo hutaki tundu ndani yako! Nasi tutakutupa utoke hapa, tutoroke.”

76 Kasema, “Hamwezi kwenda popote. Mtashikwa. Ninyi vijana waambie sikuhusika. Si—sikutaka kufanya jambo hili. Ni—nilikuwa nimeketi hapa. Sina hatia.” Na kwenye wakati huo polisi wakawashika.

77 Walijitetea. Akasema, “Kwanza nilimdhania wakili wa mashtaka maovu, kwa sababu yeye alisema . . . ” Haya hapa maswali aliyouliza. “Je! gari hili ni la kwako?”

Akasema, “Naam, bwana. Lakini mimi . . . ”

78 Akasema, “Jibu maswali yangu.” Loo, ndugu, ibilisi ana njia ya kufanya jambo hilo. Kasema, “Jibu maswali yangu.” Kasema, “Je! gari hili ni lako?

Akasema, “Naam, bwana.”

“Je! ile ni namba ya leseni yako?”

“Naam, bwana.”

Akasema, “Ulikuwa huko kwenye ile sehemu ya kuegeshea magari?”

Akasema, “Vema, nakwambia . . . ”

Akasema, “Jibu maswali yangu.”

Akasema, “Naam, bwana.”

79 Akasema, “Haya basi.” Na kwa ushuhuda wa hali ya mambo ilivyokuwa, walimpa miaka kumi, wakawahukumia hao vijana wengine kifungo cha maisha.

80 Sasa, akasema, "Unaona, ndugu, nilijiingiza tu katika kundi baya. Hakuna mtu wa kulaumiwa ila mimi." Na hiyo ni kweli. Sasa, ana miaka kumi, ya kutolea presha. Nilimwombea. Ndugu Wood pale, na mimi, tulikuwa tumeketi huko nje majini. Ndipo nikamshika mvulana huyo mkono, na kumwombea, huko nje majini, ya kwamba Mungu atampa kifungo cha nje. Na ningali ninamwombea, kwamba Mungu atampa.

81 Ni kitu gani? Presha, asiye na hatia, mtu asiye na hatia. Sasa, mtu huyo anapaswa kupewa nafasi.

82 Sasa, kama unataka kutenda haki, nina furaha sana, usiku wa leo, kukwambia ya kwamba kuna mji wa kukimbilia. Huo ni Yesu Kristo. Kama hutaki kufanya makosa, adui anakuandama, basi kuna njia ya kuepukia, na kuepukia huko ni Yesu Kristo. Hapo ndipo mahali unapoweza kuja na kutolea mvuke. Bali kama unapenda kutenda dhambi, wala humtaki Mungu, basi adui atakushika mahali fulani. Huna . . . Huwezi kumjia Kristo, kwa kuwa hutaki kuja.

83 Na wakati mtu huyu anapomjia Kristo, mahali hapa pa kukimbilia . . . Wakati mtu alipoingia, katika Agano la Kale; jambo la kwanza, ilimbidi aje kwa hiari yake mwenyewe. Na hivyo ndivyo inavyokupasa kumjia Kristo.

84 Jambo lingine, huna budi kuridhika wakati ukiwa pale. Huninii . . . Huwezi kutangatanga kila siku, ukilia, "Ningetaka kutoka hapa. Ningetaka kutoka hapa." Wangekufukuza. Huna budi kutaka kukaa kwa hiari yako. Inapaswa kuwa kwamba lazima uwe unataka kukaa kwenye mji huo.

85 Na unapomjia Kristo, huwezi kuangalia nyuma kwenye ulimwengu. Biblia ilisema, "Mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kulima." Sasa hapo ndipo wengi sana wanaojidai kwamba ni Wakristo wanapofanya kosa lao. Unaona, wanajifanya kana kwamba watalima, lakini jambo dogo la kwanza likitukia, wanalipuka, juu ya jambo hilo.

86 Hivi majuzi nilipatwa na tukio la jambo hilo, kama nyote mjuavyo. Nami ninawashukuru kwa ajili ya maombi yenu. Ninapowinda, na kuvua samaki, na kulenga shabaha, na kadhalika, daima nimetamani bunduki kubwa ya Weatherby. Vema, baadhi ya marafiki zangu wangelininunulia hiyo. Ninawajua watu, kama ningaliitaja tu, wangeninunulia kwa furaha. Kwa kweli, wawili ama watatu walitaka kufanya hivyo. Lakini nisingetaka kuwaona wakiweka kiasi hicho kikubwa cha pesa kwenye bunduki, wakati ninawajua wamishenari wasio na viatu miguuni mwao. Nisingeweza kufanya jambo hilo. Ndipo Ndugu Wilson akampa Billy Paul Roberts .257 ndogo. Na ndugu mmoja, rafiki yangu akasema, "Ndugu Branham, Weatherby wanaweza kutoboa shimo kwenye bunduki hiyo, ninaweza kuitengeneza kwa bei rahisi, kama utaniruhusu nikufanyie jambo hilo." Vema, nilimruhusu alifanye.

87 Nikarudi, nikaweka risasi kwenye bunduki hiyo, na nikaanza kupiga bunduki, na kitu hicho kikalipukia mikononi mwangu. Ndipo mtutu ukarushwa karibu kwenye ile laini ya yadi hamsini, komeo huko nyuma yangu kabisa. Na ni ajabu haikunikata tu vipande viwili. Kulikuwa na kama tani tano au sita za presha karibu *sana* na mimi.

88 Vema, daktari alisema, "Jambo pekee nijualo, ni kwamba Bwana mwema alikuwa ameketi pale kumlinda mtumishi Wake."

89 Sasa, jambo ninalofikiria, hapa ndipo linapotokea. Laiti hiyo ingalikuwa ni Weatherby kubwa, kwa kuanzia! Shida ilikuwa nini? Kulikuwa na kasoro kwenye bunduki hiyo. Nafasi ya kichwani ilikuwa imetobolewa legevu sana. Hiyo ndiyo shida kwa wengi wetu katika wongofu wetu, nafasi yetu ya kichwa imetobolewa legevu sana.

90 Na—na, sasa, kama hiyo ingalikuwa ni Weatherby, tangu mwanzo, tangu ile feleji iliyomiminwa, kutengeneza mtutu wake, ingelikuwa imetobolewa na kufanywa Weatherby Kubwa, haingelipuka. Lakini kwa sababu walijaribu kuibadilisha kuwa kitu ambacho kwa kweli haikuwa, basi ililipuka.

Na vivyo hivyo kila mtu atapata jambo lile lile, ambaye anakiri kuwa Mkristo, ambaye hapati msingi mzuri tangu kule Kuzaliwa kupya, atalipukia mahali fulani. Kuna presha nyingi kupita kiasi kwake. Haitastahimili. Atajikuta amelipuliwa mahali fulani.

91 Watu wakijaribu kuigiza huduma ya mtu fulani, ambayo hawajaitiwa, hatimaye italipuka. Huna budi kuchaguliwa na Mungu.

Haina budi kuwa ni Mungu, si kupeana mkono kidogo, hadithi fulani ya kuvutia akili, bali ni kuja kwa msingi wa Damu ya Kristo iliyomwagika, na imani yako katika yale Mungu aliyokufanyia kupitia Yesu Kristo. Kama sivyo, utalipuka mahali fulani. Mtu fulani atakanyaga vidole vyako, nawe huyoo utalipuka. Unaona? Unaona, ni kulundikana kwa presha, wakati wote, na karibuni italipuka.

92 Mtu huyo hana budi kuwa anataka kukaa katika kimbilio. Hawezi kuingia kule akilalamika. Hana budi kutaka kukaa, pasipo kulalamikia jambo hilo. Nje, yeye anakufa. Ndani, yeye ni salama.

93 Vema, ninataka kusema jambo fulani, watu hapa, kama wewe si Mkristo. Nilikuja kwenye mji huu wa Kimbilio, kama miaka thelathini na moja iliyopita. Na, ndugu, sijataka kamwe kutoka. Loo, niliingia ndani ya Kristo. Kila kitu nilichotamani kilikuwa *Hapa* ndani. Sitaki kutoka. Ninaomba kila siku, "Ee Mungu, nina furaha sana hapa. Nijalie tu nikae." Kamwe sitaki kuondoka, nami ninajua Yeye hataniacha kamwe. Ninajua hatakuacha kamwe. Na presha inaongezeka, kama ikiongezeka,

basi Yeye ndiye mahali petu pa kuitolea, kwa hiyo haitupasi ku—kuhangaika kuhusu hilo.

94 Kama umeshinikizwa kabisa, wala hujui unakoenda, itakuwaje kwako baada ya kifo; nawe unajua utakufa siku moja, huna budi kufa; basi jambo la kuja, ni kumjia Kristo, yule Kimbilio, na kutoa presha. Amua, mara moja.

95 Haidhuru ni jambo gani litakalotukia, Kristo ndiye Kimbilio letu. Na tunapomjia, tunaweza kutoa presha. Unaweza kuacha kufadhaika kuhusu, "Vema, kama nikifa, itakuwaje kwangu? Itakuwaje kwa mke wangu? Itakuwaje kwa mume wangu? Itakuwaje kwa watoto wangu?" Mjie tu Kristo, na utoe presha. La, Yeye ametupa vitu vyote. Vitu vyote ni vyetu, kwa Kristo, kwa hiyo achilia tu presha itoke, njia moja pekee unayoweza kulifanya.

96 Mtu fulani anaweza akakupa dola milioni moja. Ingepandisha presha.

Unaweza ukajiunga na kanisa, na bado ingepandisha presha. Maana, Wamethodisti watakwambia wao ni sahihi, "Na Baptisti si wa kweli." Naye Mbaptisti atasema, "Wamepotoka, na sisi ndio sahihi." Kwa hiyo inapandisha tu presha zaidi, maana hujui unakosimama.

97 Lakini kama ukiwahi kumjia Kristo, unaweza kutoa presha, kwa sababu yote yamekwisha basi, amua tu. Ndipo mahali palipoandaliwa na Mungu pa usalama, ambapo Mungu alisema, "Jina la Bwana ni ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama."

Katika wakati wa ugonjwa, wakati ugonjwa unaposhambulia, na daktari anasema, "Sina lingine ninaloweza kufanya juu ya jambo hilo," usipandishe presha.

Toa presha. Mwite mchungaji wako. Acha akupake mafuta na kukuombea. "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa yule." Toa presha. Unaona?

98 Yeye ndiye Kimbilio letu. Unapokuwa kwenye Kimbilio hili, una—una haki ya kitu chochote kilicho katika Kimbilio hili. Na Kristo ndiye Kimbilio letu, na kila unachohitaji kimo ndani Yake. Amina.

Katika ugonjwa, usipandishe presha. Toa presha.

99 Unasema, "Vema, na—nashangaa, Ndugu Branham." Usishangae; toa tu presha. Kabidhi shida yako kwa Mungu, na uendelee kana kwamba yote yamekwisha. Usipandishe presha. Inatoa presha.

100 "Vema," unasema, "Nina wasiwasi sana, Ndugu Branham. Sijui kabisa."

Toa presha. Amina. Katika mji wa Kimbilio, Yeye alichukua wasiwasi wako, kwa hiyo ha—haikulazimu kuwa nao. "Mtwike

Yeye fadhaa zako, kwa maana Yeye hujishughulisha sana na mambo yako.” Usijali juu ya fadhaa zako. Hiyo ni kazi Yake.

101 Nilikutana na mwanamke mmoja, hapa miaka kadhaa iliyopita kwenye duka la senti kumi. Alikuwa na umri wa karibu miaka sitini, alionekana mwenye umri wa kama miaka thelathini. Nikasema, “Umefanikiwaje, dada?”

102 Akasema, “Ndugu Branham, nina wana wawili ambao ni madaktari, ambao wana umri mkubwa kuliko wako.” Na kwa kweli, ha—hakuonekana mwenye umri wa zaidi ya miaka thelathini. Akasema, “Mambo yalikuwa hivi. Nilipomjia Kristo, wakati nilipokuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, niliketi chini na kuwazia jambo hilo. Nilichunguza dini zingine. Lakini wakati nilipoona iliyo ya kweli,” akasema, “nilimjia Kristo, na nikapeleka jambo langu, nafsi yangu, yote niliyo, Kwake.” Kisha akasema, “Sijapata kuwa na fadhaa tangu wakati huo.” Kasema, “Sasa, Yeye aliahidi kushughulikia shida zangu zote,” tena kasema, “kama Yeye si mkubwa vya kutosha kuzishughulikia, ninajua mimi si mkubwa vya kutosha kuzishughulikia, basi kuna faida gani mimi kufadhaika juu ya jambo hilo?” Unaona? Jambo ndilo hilo.

103 Kristo aliahidi ya kwamba angeshughulikia fadhaa zako zote. “Mtwike fadhaa zako.” Kwa hiyo unafadhaika kitu gani? Fadhaa hupandisha presha. Presha hulipuka. Kwa hiyo mtwike tu fadhaa zako, na uache kufadhaika. Vema.

104 Sasa, “Vema,” unasema, “nitafanyaje jambo hilo?” Amini tu ahadi Yake. Yeye alitoa ahadi ya kwamba angefanya hivyo, hata katika wakati wa kifo, hapo malaika wa mauti anapoingia chumbani. “Loo, Ndugu Branham, ninajua nitashikwa na wasiwasi.” Loo, la. Wewe uko kwenye Kimbilio. La, la. Unajua utakufa; huna budi kuondoka kwa njia fulani, kwa hiyo ingia tu kwenye Kimbilio, jisikie salama. Hiyo ni kweli. Uko salama mradi tu uko kwenye Kimbilio. Kumbuka, Yeye alikufa kwa ajili yako. Anakushughulikia. Alikufa kwa ajili yako.

105 Sasa hebu tuangalie. Unasema, “Ndugu Branham, unamaanisha, wakati malaika wa mauti anapobisha mlangoni, bado hupaswi kupandisha mvuke?” La, hata kidogo. “Vema, unafanyaje jambo hilo?” Njoo kwenye Kimbilio. Hivyo tu. “Vema,” unasema, “Ndugu Branham . . . ”

106 Vema, sasa ngoja kidogo. Hebu na tuwachukue Israeli, huko chini Misri. Ulifikia wakati ambapo Mungu alisema, “Nitamtuma malaika wa mauti apitie nchini, nami nitamchukua kila mmoja wa vifungua mimba vya familia, isipokuwa pawe na damu mlangoni,” ule usiku mkuu wa pasaka.

107 Sasa, hawa hapa Israeli, watu wa ahadi wakielekea kwenye nchi ya ahadi. Na wao walininii . . . Ni usiku wa pasaka. Malaika wa mauti yumo nchini. Nasi tunasikia kilio kikitoka huko chini barabarani. Tunaangalia nje. Mabawa mawili makubwa,

meusi, yanapigapiga barabarani. Unadhani Israeli walishikwa na taharuki hata kidogo? La, bwana.

108 Mauti ilikuwa mlangoni. Maskini mvulana mdogo aliangalia nje ya dirisha. Yeye ni kifungua mimba cha familia. Anamwona malaika huyo mkubwa mweusi. Anaangalia na kusema, "Baba, je! unanipenda?"

"Hakika, mwanangu, ninakupenda."

"Vema, Baba, hivi mimi si kifungua mimba chako?"

"Naam, wewe ndiwe, mwanangu."

"Angalia *kule*, baba. Yule malaika alimwua yule mvulana mdogo. Nilimjua. Nilicheza naye. Loo, baba, huyu hapa anakuja, akielekea huku nyumbani."

"Lakini, mwanangu, je! unaona kwenye kile kizingiti cha mlango?" Haleluya!

"Baba, ataniua?"

"La, bwana, mwanangu. Hawezi kukuua."

"Kwa nini?"

109 "Hiyo ni ahadi Yake. 'Nitakapoiona hiyo Damu, nitapita juu yenu.' Rudi ukachukue wanasesere wako, na uanze kucheza, mwanangu. Hakuna haja ya kufadhaika. Sisi tuko katika kimbilio la Mungu. Toa mvuke."

110 Israeli wangeweza kuketi kitako na kusoma Biblia; wakati hao wengine walipokuwa wakipiga mayowe na kupandisha mvuke, Israeli walikuwa wametulia. Kwa nini? Mauti moja kwa moja mlangoni, ilileta tofauti gani? Haiwezi kuwadhuru.

111 Kwa hiyo wakati mauti yanapokuja mlangoni mwetu, utukufu kwa Mungu, mradi tu matakwa ya Mungu, ile Damu, imewekwa kwenye kizingiti cha nguzo ya moyo wangu, inaleta tofauti gani? Haiwezi kunisumbua.

112 Daktari anasema utakufa kesho, inaleta tofauti gani? Ile Damu iko kwenye nguzo. Huna budi kufa, kwa vyovyote vile. Lakini kama Damu hiyo imepakwa, nina ufufuo unaokuja. Amina.

113 Israeli wangeweza kutulia, hawapandishi mvuke, kwa maana walijua ya kwamba malaika wa mauti asingeweza kuwapiga. Walikuwa chini ya damu. Ilikuwa ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu.

114 Sasa angalia. Wasema, "Je! ninaweza kuhakikishiwa jambo hilo?" Sasa, enyi Wakristo, hili hapa. "Je! ninaweza kuhakikishiwa jambo hilo?" Nilizungumza juu ya jambo hilo, Jumapili iliyopita usiku.

115 Sasa, Israeli walikuwa ni watu wa ahadi, wa agano, wa Mungu. Walikuwa wameahidiwa nchi iliyojaa maziwa na asali. Kwa hiyo wa—walikuwa bado hawajaiona hiyo

nchi. Hakuna hata mmoja wao aliyepata kuwa huko. Lakini walikuwa wameahidiwa hiyo. Unaona? Hawajapata kuwa huko. Hawakujua lolote kuhusu nchi hiyo, bali waliahidiwa nchi hiyo. Ndipo wakatoka kwenye utumwa wao, kwa mkono wa Mungu kupitia kwa nabii Wake, nao walikuwa ni wasafiri, wakikiri ya kwamba walikuwa ni wasafiri na wageni, na walikuwa wakielekea kwenye nchi ambayo hawakuwa wameiona kamwe, ama hakuna mmoja wao aliyepata kuiona. Wazia jambo hilo.

Kwa hiyo wakakaribia mpakani. Kulikuwa na shujaa mashuhuri miongoni mwao, jina lake Yoshua. *Yoshua* linachukua . . . linamaanisha "Yehova Mwokozi." Naye Yoshua akavuka Yordani, akaingia kwenye nchi ya ahadi, kisha akarudi na thibitisho ya kwamba ilikuwa ni nchi nzuri. Walinunua kichala cha zabibu; kilihitaji watu wawili kukibeba. Ilikuwa ni vile vile hasa Mungu alivyosema ilikuwa. Ilikuwa imejaa maziwa na asali. Hilo lilipaswa kumfanya kila mmoja wao kufurahi. Kwa nini? Yoshua alirejesha thibitisho la nchi ambayo hakuna mtu aliyejua habari zake, ambayo Mungu alikuwa ameahidi kuwapa. Unaona? Maana, walikuwa wamepata ahadi ya nchi fulani, nao walikuwa njiani kwenda huko.

116 Sasa, siku moja jamii ya binadamu ilikuwa kwenye mtego, na ndipo Mtu fulani akaja duniani, Jina Lake Yesu Kristo. *Yesu* maana yake ni "Yehova Mwokozi." Naye akashuka akaenda kwenye Yordani ya mauti. Akavuka Yordani, katika mauti, na akafufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, akiwa na ushuhuda ya kwamba mtu anaweza kuishi baada ya kufa. Haleluya! Mauti siyo mwisho. Yesu alithibitisha jambo hilo, ya kwamba mtu anaweza kuishi baada ya kufa.

117 Alisimama mbele yao, Naye akasema, kabla hajaondoka. Yeye alisema, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Kama sivyo, ningaliwaambia. Nami nitaenda kuwaandalia mahali. Nitaenda huko na kutayarisha mahali, kisha nirudi, na kuwapokea Kwangu; ili nilipo, nanyi muwepo pia." Kwenye asubuhi ya Pasaka, baada ya . . .

Yeye alikufa, mpaka mwezi na nyota na jua vikajionea aibu. Yeye alikufa, mpaka askari wa Kirumi akauchoma moyo wake kwa—kwa mkuki, ndipo maji na damu yakatengana. Alikuwa mfu aliyekufa kuliko wafu wote. Alienda kaburini, kama mwanadamu yeyote alivyofanya. "Nafsi yake ikaenda kuzimu," kama Biblia ilivyosema.

Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, Yeye alirudi kutoka mautini, kuzimu, na kaburi, na kusema, "Mimi Ndiye niliyekuwa nimekufa, Nami ni hai milele na milele, na nina funguo za mauti na kuzimu. Mimi ni Mwanadamu."

Wao walisema, "Yeye ni pepo."

Kasema, "Nipeni sambusa ya samaki." Naye akala samaki na mkate.

118 Alikuwa Mtu aliyekufa na akaenda kwenye ile Nchi, kisha akarudi na ushahidi ya kwamba mwanadamu anaweza kuishi baada ya mauti. Mauti ina uhusiano gani nasi? Amina. Toa presha.

119 Sasa, si hivyo tu, bali Yeye alitupa ahadi. Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alitupa bayana ya urithi wetu. Alisema, "Sasa kuthibitisha jambo hili kwa kila mwaminio. Sasa mnatembea hapa chini katika kutokuamini. Hamwamini Neno. Mnatembea katika dhambi na mambo ya ulimwengu. Lakini yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa Milele, Uzima usioweza kufa."

120 Angalia sasa, tunapompokea Roho Wake, sisi ambao wakati mmoja tulikuwa tumekufa katika dhambi na makosa, Yeye hutupa Kuzaliwa kupya, Uzima mpya. Anafanya nini? Yeye... Tunakufa na tunazikwa katika Yesu. Tunafufuka katika Roho, kutoka katika mambo ya ulimwengu, kuingia katika mambo ya Mbinguni. Na usiku wa leo, "Tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu."

121 Ni Wakristo wangapi hapa ndani ambao wangali wanaipenda dunia? Kama unaipenda, wewe si Mkristo. Wewe unakiri Ukristo, wala hujaumiliki. Kwa maana mtu akiisha mara moja tu kumwonja Kristo, yeye amekufa kwa mambo ya dunia, wala kamwe hana tamaa ya kuyarudia hayo.

122 Inafanya nini? "Yale maisha," Paulo alisema, "niliyoishi wakati mmoja, siyaishi tena. Hata hivyo mimi ni hai, si mimi, bali Kristo ndani yangu." Kwa nini? Yeye alimwinua kutoka kwenye kiwango hiki cha chini cha dhambi ya ulimwengu, akamwinua hadi mahali ambapo sisi wenyewe tunaweza kuangalia nyuma na kuona mahali tulipotoka. Utukufu! Kuangalia nyuma na kuona mahali ambapo tuliishi wakati mmoja. Sasa tunaishi kinyume chake. Ni kitu gani? Ni yakini ya kwamba sisi tumekufa, na maisha yetu yamefichwa katika Kristo, kwa Mungu, na tumetiwa muhuri na Roho Mtakatifu, na kuinuliwa juu ya mambo hayo. Ndipo sisi ni hai, tukiwa na ushahidi ule ule aliorudi nao, kututhibitishia.

123 Nchi hii ni nzuri sana na haya ndiyo malipo ya kwanza. Hii ni bayana ya wokovu wetu. Ndizo pesa za kwanza zinazoshikilia mapatano. Utukufu! Inashikilia mapatano ya Mungu, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, ambaye anamwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Toa presha, ndugu. Naam, bwana. Amina. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

124 Angalia, kama vile Eliya yule nabii mkuu, mfano wa Kristo. Elisha, ule mfano wa Kanisa, ambaye, sehemu maradufu ya Roho ilimjia nabii huyo. Yeye alienda hadi Yordani siku moja; mfano wa siku hii, serikali hii na mambo tuliyo nayo sasa; Ahabu, Yezebeli, na kadhalika. Kama mnavyokumbuka,

somo langu la Yezebeli. Angalieni wakati Elisha alipomfuata Eliya, kwa sababu fulani. Amina. Alimpeleka wapi? Yordani; mpaka Ramothi-Giliadi, mpaka kwenye shule ya manabii, kisha akashuka kwenda Yordani. Hivyo ndivyo anavyokupeleka. Kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, na kufa, kupokea Uzima. Amina. Si kwenye madhehebu fulani wala kanuni fulani za imani. Bali hadi kwenye mauti kwa roho yako, upate kuzaliwa mara ya pili. Naye Elisha . . .

125 Eliya aliyapiga yale maji, akavuka Yordani, naye Elisha akamfuata. Ndipo Elisha aliporudi kwenye nchi hiyo tena, ng'ambo ya pili, alirudi akiwa na sehemu maradufu.

Leo, tunamfuata Yesu hadi kwenye mauti Yake, mazishi na ubatizo. . .mauti, mazishi, na kufufuka, hasa, kupitia ubatizo. Tunamwamini. Tumeyafia mambo ya ulimwengu, tukakiri ya kwamba sisi si kitu, tukabatizwa katika Jina Lake, tukazikwa pamoja Naye katika ubatizo, tukafufuka pamoja Naye katika ufufuo. Roho zetu zinaishi juu ya mambo ya dunia. Ndipo tumo ndani ya Kristo. Sasa tuna sehemu moja.

126 Tunaporudi kutoka kwenye mstari wa mauti wa Yordani, tutakuwa na sehemu nyingine. Miili tuliyo nayo sasa, pamoja na roho tulizo nazo, ina Arbuni, Roho Mtakatifu ambaye hawezi kufa, kwa sababu Yeye ni sehemu ya Mungu. Na miili tunayoishi ndani yake. . . "Yeye aulaye mwili Wangu na kunywa Damu Yangu yuna Uzima wa milele, Nami nitamfufua katika siku ya mwisho." Amina. Toa mvuke.

127 Inaleta tofauti gani, bomu za atomiki ama chochote kile kikipiga? Hebu wafanye lolote . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .ya jambo hili moja, ya kwamba tuna Uzima wa Milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Kwa hiyo tunajali nini kuhusu yale ulimwengu utasema. Tunajali nini kuhusu presha. Haileti tofauti yoyote kwetu. Kwa nini? Kwa sababu tunaweza kutoa mvuke.

> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]
> Njoo ambapo matone ya umande wa rehema
> yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na. . .[Sehemu tupu
> kwenye kanda.]
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

128 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na tuinue mikono yetu.

> Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri,
> Njoo ambapo matone ya umande wa rehema
> yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

129 Baba yetu wa Mbinguni, Shetani ameshindwa vita. Iweni tu na subira. Msipandishe mvuke. Nikisimama hapa, nikihubiri

juu ya "kutoa mvuke," na halafu Shetani alidhani ya kwamba angeweza kunitoa mimbarani, aniondoe kwenye wito huu wa madhabahuni. La, Bwana. Ndani ya moyo wangu kulikuwa na kitu kilichokuwa kikiwaka moto, kikisema, "Yupo mtu hapa. Kuna mtu anayeutafuta ule Mwamba." Tunakushukuru, Baba, kwa ajili ya ushindi. Wakati mtu yule wa mwisho alipoenda madhabahuni, taa ziliwaka. Aliona alikuwa ameshindwa, kwa hiyo ni afadhali ajisalimishe vita.

130 Hawa hapa wamesimama, usiku wa leo, namba hiyo ya neema, watu watano wa thamani. Tano: J-e-s-u-s, i-m-a-n-i, neema, n-e-e-m-a. Ee Mungu, Wewe ni Mungu. Hushindwi kamwe. Wewe daima uko sahihi.

131 Ninaangalia, akisimama hapa upande huu hapa, binti ya Dada Wilson. Ninaweza kumkumbuka msichana huyo mdogo. Ninakumbuka wakati ulipomwita. Ninakumbuka ule usiku kwenye Soko Jipya, miaka mingi iliyopita. Kule chini usiku ule, ninakumbuka, Bwana.

132 Huyu hapa amesimama karibu naye, mama mmoja, ameshuka kuja kutoka New York, kututembelea.

133 Huyu hapa kijana mwanamume na kijana mwanamke, kwenye wakati huu tu wa kuamua, wakati walimwengu wako huku nje wakifanya kila namna ya madansi machafu na kufanya yasiyofaa. Wametembea, wakiutafuta ule Mwamba.

134 Mwishoni mwa madhababu yale amesimama kijana, mikono yake imeinuliwa, a—anataka kuupata ule Mwamba. Yesu, Wewe ndiwe ule Mwamba. Nawe ulisema hivi, "Popote wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Basi, Mwamba huo upo papa hapa.

135 Linaweza kuonekana ni jambo geni sana, Baba, rahisi sana. Unayafanya mambo kuwa rahisi sana, kusudi tusikosee. Lakini kwa kuwa waliamka kutoka kwenye viti vyao na wakaja kwa mwaliko; kwa maana, kwamba, Shetani alijaribu kuwafanya wasije, kila jitihada aliyoweza kufanya, alijaribu kufanya hivyo, bali alishindwa. Sasa, kama mtumishi Wako, ninawawekea mikono yangu, na kutangaza baraka Zako. Na, Mungu, jalia zifuate. Kwa kuwa kwamba wao ni waaminifu na wanyofu kufuata mwongozo wa Roho, ninafanya vivyo hivyo.

136 Sasa, ninaomba ya kwamba nafsi ya dada yangu haitaangamia kamwe, ya kwamba atapewa shauku ya moyo wake kwa ajili ya Uzima wa Milele, katika Jina la Yesu Kristo.

137 Ninaweka mkono wangu juu ya dada yangu, na ninajua ya kwamba majaribu mengi yamemkumba. Ninajua ya kwamba anamwombea mvulana wake mpendwa. Ninamjua baba yake, wakati machozi yakitiririka mashavuni mwake, usiku wa leo, wakati alipokuwa akiwasilisha ile sehemu ndogo ya fungu la kumi. Na asubuhi ya leo, wakati tulipoomba na kumkabidhi mvulana huyo kwa Bwana Mungu. Mama huyu na baba

wanampenda mtoto huyu. Na, Mungu, wanataka mahali ambapo wanaweza tu kutoa mvuke na kujua ya kwamba kila kitu ni shwari. Baba, tumelikabidhi Kwako. Utatujalia. Hatuna hofu. Mpe hakikisho hilo sasa hivi, Baba, katika Jina la Yesu ninaomba.

138 Na, Baba, kijana mwanamume huyu na mwanamke wamekuja pamoja, kwa hiyo ninaweka mikono yangu juu yao. Wamekuja kutoa mvuke. Mume na mke vijana namna hii, vijana warembo, tunajua wao ni chambo halisi cha ibilisi kama angeweza tu kuwatumia. Bali wamenyakuliwa, kama kinga cha moto. Wamekuja kwa maana wanataka kupata kimbilio hilo. Wanataka kufikia mahali ambapo wanaweza tu kutoa mvuke, kutoa presha, wajitulize mbele za Mungu, na kujua ya kwamba Yeye ni Mungu. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawapa ile hakika iliyobarikiwa sasa hivi. Jalia kila ganda dogo liondolewe, sasa hivi.

139 Jamaa huyu mdogo hapa, Bwana, anayesimama ameinua mikono yake juu, huyo wa mwisho kabisa. Na mara alipoamka akaja huku, taa ziliwaka. Hiyo ndiyo idadi uliyotaka, huo ulikuwa ndio wito Wako. "Wote alionipa Baba watakuja." Jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kulishikilia Neno pale, na hao Baba aliowakusudia Uzima watafuata. Na sasa amekuja. Anataka kupata ule ufa, Bwana, kusudi aweze kuketi chini na kupumzika kidogo. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utamwongoza kwenye huo ufa sasa hivi.

140 Jalia kila pingu ivunjwe. Jalia kila kitu, kila kipingamizi ambacho kimemsumbua yeyote wa hawa, jalia kianguke kutoka kwao sasa hivi; jalia kile kitu kidogo, hasira ndogo, kitu kidogo chochote kile, hasira ndogo ya haraka, ule wasiwasi mdogo, ile tashwishi, ile dhambi ndogo ituzingayo. Bwana, kama ndugu yao, na mtumishi Wako, ninawaombea dua, kama kusimama kati ya walio hai na waliokufa. Mungu, ninadai nafsi zao. Ninadai ushindi wao, katika kutii wito wa madhabahuni. Nasi tunajua ya kwamba Shetani alijaribu kuuzima. Lakini tunawadai, ninawadai sasa, kama mtumishi Wako. Nami ninawakabidhi kwa Yesu Kristo, kama tuzo za neema Yake, tuzo za Uwepo wa Roho Mtakatifu, usiku wa leo, ambaye aliwaita chini ya hali ngumu, na kuwaleta kwenye ule Mwamba. Jalia washushe presha sasa, na wajue ya kwamba Yesu alisema, ya kwamba, "Hakuna mtu awezaye kuja mpaka Mimi nimwite. Na wote wajao, nitawapa Uzima wa Milele, na kuwafufua katika siku ya mwisho." Imekwisha, Bwana. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

141 Mungu awabariki, mnaposimama hapo. Mnaporudi kwenye viti vyenu, nendeni na mjue ya kwamba kila kitu mlichowahi kuonea shauku, na kila dhambi iwazingayo na kitu kilichokuwa kibaya, kiko chini ya ile Damu. Imekwisha. Je! *wewe* unaamini? *Wewe* unaamini? *Wewe* unaamini, ndugu? *Wewe* unaamini, dada?

Wewe unaamini? Basi, si—si *itatendeka*; *imetendeka*. Hiyo ni kweli. Ni wakati uliopita.

142 Mungu awabariki, yaliyo bora kabisa katika maisha na Uzima wa Milele, ambao mnao sasa. Mmepanda juu, juu ya dhambi. Dhambi iko chini ya miguu yenu. Itanifaidi nini, kusimama hapa, kuwaambia jambo lisilo kweli? Ningehesabiwa mdanganyifu mwishoni mwa safari. Unaona? Mmepokea Uzima wa Milele, kwa maana mlimwamini Bwana Yesu Kristo. Sasa mkiweka kando kila dhambi na kila pingu, iweni huru. Toeni mvuke. Wewe ni Mkristo. Umeinuliwa juu ya dhambi. Una arbuni ya wokovu wako wa Milele kwa kuwa Kristo amekupokea.

143 Sasa, hivi Yeye hakusema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wanijiao, nitawapa Uzima wa Milele na kuwafufua katika siku za mwisho"? [Hao watano madhabahuni wanasema, "Amina."—Mh.] Basi imekwisha. Amina. Yote yamekwisha. Mungu awabariki sasa, na awe mwenye rehema kwenu.

Je! mnampenda, huko mliko? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

144 Ni wangapi wanaojisikia presha yote imekwisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

> Nimetia nanga nafsi yangu katika kimbilio la
> raha,
> Sitaabiri bahari zenye tufani tena;
> Tufani zaweza kupitia juu ya vilindi vyenye
> dhoruba,
> Lakini katika Yesu mimi ni salama milele.

145 Ni kama hadithi ya Charles Wesley, akiwa mahali pake pa faragha huko kando ya bahari siku moja, alikuwa na kibanda kidogo. Alikuwa akisoma. Bwana alimwongoza kule chini. Alikuwa akisoma. Loo, Mungu alikuwa akitenda kazi ndani yake, apate kutunga wimbo. Wala asinge—asingepata chochote cha kuanzia. Angeanza na jambo fulani, uvuvio ungemwacha. Kwa hiyo akaenda akitembea ufukoni mwa bahari, akiyasikiliza mawimbi, na akafikiri angepata uvuvio fulani, mawimbi yakipiga. Mara, ikatokea dhoruba.

Hakuna jambo linalotukia kwa bahati. Kila kitu kimeamriwa na Mungu. Haidhuru jambo gani linatukia, mambo yote yatatenda kazi kwa manufaa.

146 Basi akaanza kwenda kwenye kibanda chake kidogo. Alipofanya hivyo, pepo zilianza kuvuma. Akawazia, "Loo,

nitapeperushwa kutoka hapa, u—ufukoni, kabla sijafika kule." Ndipo akajifunika kwa koti lake, akaanza kukimbia, ndipo kitu fulani kikaruka kikagonga kwenye kifua chake. Akaangalia nyuma, na ilikuwa ni shomoro mdogo, akija kujificha. Alimshikilia tu kifuani mwake mpaka dhoruba ilipokwisha, na jua likachomoza. Akamweka maskini jamaa huyo juu ya kidole chake, akamwacha aruke aende zake. Naye akaruka akaenda zake, ndipo uvuvio ukamgusa.

Mwamba wa Kale, uliopasuliwa kwa ajili yangu,
Kwako nitajificha.

147 Loo, ninaupenda huo! Mwamba wa Kale, ule Mwamba katika nchi yenye uchovu, Kimbilio wakati wa dhoruba. Unaona? Mwamba huo katika nchi yenye uchovu, nifiche mimi. Nifiche, Ee Mwamba wa Kale, uliopasuliwa kwa ajili yangu. Wale watunzi mashuhuri wa nyimbo waliovuviwa na kadhalika tunazofurahia sana siku hizi!

Unasema, "Ati nyimbo hizo zimevuviwa?"

148 Yesu alizirejea wakati alipokuwa hapa duniani, alisema, "Haikuandikwa katika Zaburi, Daudi alisema jambo *fulani*?" Hakika, zimevuviwa. Ni kama tu kuhubiri ama chochote kile, zimevuviwa.

149 Nina furaha sana kwamba nina Kimbilio. Sina kimbilio lingine. Naam.

Tumaini langu limejengwa si juu ya chochote pungufu
Ila Damu ya Yesu na haki Yake;
Yote yanayoizunguka nafsi yangu yakiporomoka,
Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na ngome yangu.
Kwa kuwa kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama,
Sehemu zingine zote ni changarawe ididimiayo, haidhuru ziwe ni nini.

150 Mungu awabariki. Mchungaji wenu sasa, Ndugu Ruddell. Samahani, Shetani alizizima hizo taa, bali Mungu alipata ushindi, kwa vyovyote vile. Amina.

Kutoa Presha SWA62-0513E
(Letting Off The Pressure)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 13 Mei, 1962, katika Maskani ya Injili kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org